

OFISI YA RAIS- TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

SHULE YA SEKONDARI IGIGWA,

S L P 124,

SIKONGE

Kumb. Na. HWS/IGSS/ADM/10/2021

10/12/2020

KWA

YAH; KUJIUNGA NA MASOMO YA ELIMU YA SEKONDARI KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

Nafurahi kukutarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na masomo ya elimu ya sekondari kidato cha kwanza katika **shule ya sekondari Igigwa mwaka 2021**. Shule ni ya kutwa . Ina Hosteli kwa wasichana wachache watakaopenda na kumudu ghamama zake. Shule ipo makao makuu ya **kata ya Igigwa wilaya ya Sikonge**. Mwanafunzi anatakiwa kufika shulenii tarehe **11/01/2021 saa 1:10 asubuhi** na masomo yataanza tarehe **13/01/2021**. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021** na baada ya hapo mwanafunzi/mzazi au mlezi atachukuliwa hatua za kisheria kwa kushindwa kumleta motto wake shulenii.

Ni vema mwanafunzi afikapo shulenii au kabla, akapima afya yake ili kuiwezesha shule kumhudumia kulingana na afya yake. Sheria za shule, fomu ya kujandikisha, mkataba wa mzazi/mlezi kumsomesha mwanae, fomu ya vipimo vya afya, maeneo yasiyoruhusiwa mwanafunzi kutembelea na makosa yanayoweza sababisha mwanafunzi kufukuzwa shule yameambatanishwa. Aidha, mzazi na mwanafunzi anashauriwa kusoma, kuelewa na kuzingatia barua hii na viambatisho vyake.

Mambo muhimu ya kuzingatia;

1; **SARE ZA SHULE; Wasichana;** sketi 2 zenyne malinda rangi ya damu ya mzee, shati mikono mifupi 2 (tetron), Soksi pe 3 nyeupe (stocking), Viatu vya ngozi pe 2 vyeusi visigino vifupi, nywele fupi.

2; **SARE ZA SHULE; Wavulana;** Suruali 2 rangi ya damu ya mzee (zenyne malinda mawili kila upande), shati 2 nyeupe mikono mifupi (tetroni), soksi nyeupe pe 3, viatu vya ngozi vyeusi pe 2 visigino vifupi na mikanda 2 mieusi.

NB; Hijabu iwe ni sketi ya rangi ya damu ya mzee, kilemba cheupe na shati jeupe (mikono mirefu) isiyobana mwili.

3; **VIFAA VYA MASOMO;** Daftari 10 kubwa, kalamu (biki) ya wino bluu/nyeusi 2, penseli 1, Rula 1, Mkebe wa hesabu 1, kamusi (dictionary) ya kiingereza kwa Kiswahili au kiingereza kwa kiingereza 1 (**lazima**).

4; **VIFAA VYA MICHEZO NA KAZI ZA NJE; Wavulana-** bukta ya njano, **Wasichana – Tracksuit ya bluu (Chelsea)**, suruali /sketi nyeusi kwa ajili ya kazi za nje ya darasa, T –Shirt ya bluu, Raba nyeusi kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana, (**kwanja 1, fagio 1, jembe1, na ndoo 1 ni lazima na mwanafunzi atatunza mwenywewe**)

Kwa wanafunzi watakaopenda kuishi Hosteli /shulenii, wazazi/walezi watajaza mkataba uliopo shulenii unaoonesha mahitaji muhimu. Aidha, vifaa vya malazi, chakula, na mahali pa kuishi (kwa mwanafunzi wa kutwa), mzazi/mlezi atajitafutia na atajigharamia. **Mwanafunzi wa kutwa aishi umbali kati ya 0KM – 1KM kutoka shule ilipo.**

Nakutakia maandalizi mema na karibu sana shule ya sekondari Igigwa.

.....
ISSAH S. I

MKUU WA SHULE (0627690286 / 0757969649)